

MAELEKEZO YA WN-OR (MUUUB) MHE. JENISTA MHAGAMA KWA WAAJIRI
KUHUSU UTEKELEZAJI WA AGIZO LA KUWAREJESHEA MICHANGO
WALIYOHANGIA KATIKA MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII WATUMISHI
WALIOONDELEWA KATIKA UTUMISHI WA UMMA KWA KUGHUSHI VYETI

Mnamo tarehe 27 Oktoba, 2022 nilitoa maelekezo ya Serikali ya namna ya kushughulikia watumishi wa umma walioondolewa kazini kwa sababu ya kughushi vyeti. Katika maelekezo hayo, niliwahimiza waajiri kutekeleza masuala yafuatayo:-

- a) Kutoa ushirikiano kwa watumishi walioghushi vyeti pindi wanapofika katika Ofisi zao kukamilisha taratibu za ulipwaji ikiwa ni pamoja na kuwasilisha nyaraka muhimu kwa ajili ya kulipwa michango yao walioiachanga kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii ikiwa ni pamoja na kujaza na kusaini Hati ya Ridhaa (Commitment Bond). Aidha, niliwaagiza waajiri wote kuwasiliana na Ofisi za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii za Wilaya na Mikoa ili kupata taarifa sahihi za watumishi hao zinazohusiana na zoezi hilo.
- b) Kuandaa na kuwasilisha kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hati ya ridhaa (Commitment Bond) pamoja na nyaraka nyingine kwa kuzingatia taratibu na miongozo ya Mifuko husika;
- c) Kuandaa Dawati la Msaada (Help Desk) ili kufanikisha na kurahisha mchakato wa ulipaji wa michango hiyo ikiwa ni pamoja na ujazaji wa mkataba wa makubaliano (Commitment Bond);
- d) Kuzingatia misingi ya utawala bora ikiwa ni pamoja na kuepuka vitendo vya rushwa wakati wa zoezi hili.

Pamoja na kutoa maelekezo hayo, mara kadhaa Ofisi yangu imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya walengwa wanaohusika na zoezi hili kuwa baadhi ya waajiri hawatekelezi maelezo hayo ya Serikali kwa ukamilifu na hasa kutokutoa ushirikiano katika ujazaji wa Hati ya Ridhaa (Commitment Bond) pamoja na kuchelewesha kuwasilisha vielelezo husika kwa ajili ya kuwawezesha walengwa kurejeshewa michango yao, jambo ambalo linaleta usumbufu kwa walengwa kufuatilia msamaha ambao Mhe. Rais ameutoa.

Kwa kuwa nina dhamana ya kumsaidia Mhe. Rais kusimamia masuala ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, natumia fursa hii kwa mara nyingine kuwaelekeza tena waajiri wote kuhakikisha wanatekeleza ipasavyo maelekezo ya Serikali niliyoyatoa mnamo tarehe 27 Oktoba, 2022.

Hata hivyo, kupitia Ofisi yangu, nimekwisha kuunda Timu ya kufanya uhakiki na kufuatilia mienendo ya waajiri wote katika kutekeleza maelekezo haya ya Serikali. Ninaamini kila mwajiri atatekeleza wajibu wake ipasavyo.